# NGUZO KUMI ZA KILIMO KWANZA

## (MFUMO WA UTEKELEZAJI)

## NGUZO YA 1
## DIRA YA TAIFA YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.1 | Kupitisha Dira ya KILIMO KWANZA | 1. AZIMIO LA KILIMO KWANZA | Agosti 2009 | Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Viongozi wote; Wakuu wa Taasisi, Mashirika na wa Sekta Binafsi |
| | | 2. Kuanza mpango wa utekelezaji wa KILIMO KWANZA | | | |
| | | 3. Kusisitiza utashi wa kisiasa katika ngazi zote za uongozi na nia thabiti kwa Watanzania kutekeleza Azimio la KILIMO KWANZA | Muda wote | | |
| 1.2 | Kilimo cha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa kiwe cha kisasa na cha kibiashara | 1. Kuwaendeleza wakulima wadogo na wa kati kuwa wakulima wa kisasa na wa kibiashara. | 2009 - 2015 | KILIMO | MIFUGO; MAJI; TAMISEMI; VIWANDA; ARDHI; SM; TPSF; NGOs; CBO; FBO |
| | | 2. Kuhimiza wakulima wa kati na wakubwa wachangie kwa ukamilifu kufanikisha KILIMO KWANZA | | | |

# NGUZO YA 2
# KUGHARAMIA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.1 | Kuongeza Bajeti ya Serikali kwa ajili ya KILIMO KWANZA | 1. Kutenga si chini ya asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali kwa sekta ya kilimo kwa mwaka 2010/11 na kuendelea kuongeza kiwango hicho mwaka hadi mwaka kwa bajeti zinazofuata. | Kuanzia Desemba 2009 | FEDHA | Wizara na Idara za Serikali (WIS) |
| | | 2. Bajeti za wizara nyingine zote zizingatie utekelezaji wa KILIMO KWANZA | Kuanzia Desemba 2009 | OWM | FEDHA; WIS; SM |
| | | 3. Kuwahimiza na kuwashawishi Washirika wetu wa maendeleo kusaidia KILIMO KWANZA | Muda wote | FEDHA | WIS |
| | | 4. Kuongeza Bajeti ya umwagiliaji kufikia hekta zisizo pungua milioni 7. | Ifikapo 2015 | MAJI | KILIMO; FEDHA; WAHISANI |
| 2.2 | Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). | Uanzishaji wa Benki ya Kilimo (TADB) uharakishwe ikiwa na mtaji wa kuanzia wa dola za Kimarekani millioni 500. | Desemba 2009 | BENKI KUU | FEDHA |
| 2.3 | Kutafuta mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) | 1. Kuweka mipango ya upatikanaji wa mikopo na misaada kwa ajili ya Benki ya Kilimo kutoka vyanzo vya kimataifa. | Kuanza Agosti 2009. | FEDHA | MAMBO YA NJE WAHISANI |
| | | 2. Kufanya mashauriano na benki za biashara na wadau wengine kumiliki dhamana za Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) | Kuanza Agosti 2009. | BENKI KUU | FEDHA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.4 | Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) kuwa na dirisha maalumu la mikopo ya kilimo (uzalishaji) itakayotolewa kwa masharti nafuu. | Kuongeza fedha kwenye Kitengo cha Kilimo cha Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) kuwezesha kutoa mikopo ya muda mrefu na yenye masharti nafuu kwa misingi ya viwango vya kimataifa. | Agosti 2009 | FEDHA | WAHISANI<br>Mashirika ya Fedha ya Kimataifa |
| 2.5 | Mfuko Maalumu wa Fedha kwa ajili ya KILIMO KWANZA uanzishwe | Kutafuta mtaji wa kutosha kwa ajili ya Mfuko Maalumu wa Fedha kugharimia upimaji ardhi, uwekezaji, ujengaji uwezo wa wafanyakazi na dhamana ya upatikanaji wa mikopo kukidhi mahitaji ya KILIMO KWANZA | kuanza Desemba 2009 | FEDHA | WAHISANI<br>TPSF |
| 2.6 | Kuimarisha Mfuko wa Programu ya Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo (ASDP) kutekeleza KILIMO KWANZA. | Kupanua ushiriki wa Washirika wetu wa Maendeleo katika Mfuko wa Programu ya Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo (ASDP) | Kuanza Agosti 2009 | FEDHA | WAHISANI |
| 2.7 | Kuhamasisha sekta binafsi iongeze uwekezaji katika sekta ya Kilimo kuanzia ngazi ya chini, kati na wakubwa. | Kuhamasisha sekta binafsi kuongeza uwekezaji katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA. | Kuanza Agosti 2009. | TPSF | OWM, FEDHA WAHISANI HODECT ACT, CTI, TCCIA |
| 2.8 | Kuviwezesha Vyama vya Ushirika na SACCOS viweze kutafuta, kusimamia na kuelekeza mitaji kwa wanachama wao ili kuimarisha uzalishaji katika kilimo. | 1. Kuandaa mkakati wa taifa wa kuongeza uelewa wa maswala ya fedha. | Kuanza Agosti 2009 | BENKI KUU | FEDHA; MABENKI |
| | | 2. Kuimarisha uwezo wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima na SACCOS kusimamia ipasavyo rasilimali katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | SM; NGO; CBO; FBO |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.9 | Kuandaa utaratibu wa kisheria wa kuyawezesha Mabenki ya Biashara kukopesha asilimia ya amana zao kwa ajili ya kilimo kwa masharti nafuu. | 1. Kujadiliana na mabenki ya biashara na wadau wengine kuhusu kukopesha sekta ya kilimo kwa masharti nafuu. | Kuanza Agosti 2009 | FEDHA | SHERIA; BENKI KUU; |
| | | 2. Kurekebisha kanuni na taratibu za kurahisisha utoaji mikopo ya uzalishaji katika Kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | BENKI KUU | TBA |
| | | 3. Kuhimiza na kusaidia Mabenki kuwa wabunifu wa utoaji mikopo inayolenga utekelezaji wa KILIMO KWANZA. | Kuanza Agosti 2009 | BENKI KUU | TBA |
| 2.10 | Kuimarisha uanzishaji wa Mabenki ya Wananchi katika mikoa yote ya Tanzania. | 1. Kuanzisha mabenki ya wananchi na asasi za fedha katika maeneo ya vijijini na wilayani. | Kuanza Agosti 2009. | OWM | KILIMO; TAMISEMI BENKI KUU, |
| | | 2. Kujenga uwezo wa usimamizi wa Mabenki ya Wananchi na kuimarisha chama chao. | | | |
| 2.11 | Kuanzisha vitengo maalum katika asasi za fedha kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo | Benki za Wananchi na asasi nyingine za fedha kama vile Benki ya Posta Tanzania (TPB), AZISE na taasisi za fedha kwa wateja wadogo zianzishe vitengo maalum kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | BENKI KUU | TBA; MABENKI |
| 2.12 | Kuanzisha masoko ya mazao (Commodity Exchanges) na uwezeshaji wa makampuni ya kilimo yaweze kuuza hisa zao kwenye Soko la Mitaji la Dar es Salaam. | 1. Kuanzisha Masoko ya Mazao (Commodity Exchanges) | Kuanza Agosti 2009 | CMSA | FEDHA; TPSF |
| | | 2. Kuwezesha uuzaji wa hisa za makampuni ya kilimo katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam. | | | |
| 2.13 | Mifuko ya Pensheni, Uwezeshaji na mifuko mingine ikubaliane utaratibu wa kuwekeza | 1. Kujadiliana na mifuko ya pensheni na mifuko mingine ya uwezeshaji kukopesha kwa masharti nafuu kwa ajili ya uzalishaji wa sekta ya kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | FEDHA | PSPF; NSSF; PPF;LAPF; GPF |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | asilimia ya pato lao katika uzalishaji wa sekta ya kilimo kwa masharti nafuu. | 2. Kuanzisha Mfuko wa Dira Tanzania (Vision Tanzania Fund) kwa ajili ya kukopesha sekta ya kilimo (uzalishaji). | Kuanza Agosti 2009 | FEDHA | UTT |
| 2.14 | Kuanzisha utaratibu wa malipo ya ustawi wa jamii (Social Security) kwa wakulima | 1. Kuanzisha mfuko maalum wa malipo ya ustawi wa jamii kwa wakulima<br>2. Kuhamasisha wakulima wajiunge na mifuko ya ustawi wa jamii. | Kuanza Agosti 2009 | FEDHA | TAMISEMI |
| 2.15 | Kuandaa sera na taratibu kwa ajili ya makampuni ya bima kutoa kinga ya bima na mikopo ya uzalishaji ya sekta ya Kilimo. | Kujadiliana na makampuni ya bima ili yaanzishe bima ya kinga na mikopo ya uzalishaji katika sekta ya kilimo. | Desemba 2009 | FEDHA | TAMISEMI; MAKAMPUNI YA BIMA |

# NGUZO YA 3
# MUUNDO MPYA WA TAASISI KWA AJILI YA USIMAMIZI WA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.1 | Kurekebisha muundo wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA | 1. Kusisitiza utawala bora katika sekta zote za uchumi na katika ngazi zote.<br>2. Kuimarisha Wizara ya Kilimo na kuboresha kazi za kongano ya kilimo. | Mapema iwezekana-vyo | MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | |
| | | 3. Kuingiza masuala ya mazingira katika shughuli za KILIMO KWANZA | Inaendelea | OFISI YA MAKAMU WA RAIS | WIS; SM; TPSF |
| | | 4. Kuanzisha Wakala wa Taifa wa Umwagiliaji (National Irrigation Agency - NIA) unaojitegemea chini ya Wizara ya Kilimo.<br>5. Kuunganisha mifuko miwili ya umwagiliaji chini ya Wakala wa Taifa wa Umwagiliaji (NIA). | Mapema iwezekana-vyo | MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | |
| 3.2 | Kuanzisha utaratibu wa kuratibu uhusiano na wizara nyingine zinazohusiana na maswala ya kilimo. | Kuanzisha Kamati ya Kilimo ya Baraza la Mawaziri kuratibu shughuli za wizara zote zinazohusiana na kilimo. | Mapema iwezekana-vyo | OWM | FEDHA; ARDHI; KILIMO; MIFUGO; MAJI; VIWANDA; TAMISEMI |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.3 | Kuanzisha utaratibu wa ubia wa sekta ya Umma na ya Binafsi kwa ajili ya KILIMO KWANZA | 1. Kuanzisha Tume ya Taifa ya Kilimo na Vyama vya Ushirika (National Agriculture and Cooperatives Commission - NACC) kwa ajili ya ubia wa sekta ya Umma na ya Binafsi katika kuendeleza kilimo pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA. | Julai 2010 | OWM | TPSF; |
| | | 2. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa KILIMO KWANZA | Kuanzia sasa | OWM | KILIMO |
| 3.4 | Kuimarisha Vyama vya Wakulima kwa ajili ya kuboresha ushirikiano na Serikali katika utungaji wa sera, mikakati, utekelezaji na tathmini ya utendaji kazi wa sekta ya kilimo. | Kusaidia kujenga uwezo wa wakulima na Vyama vya Wakulima katika utekelezaji wa programu za KILIMO KWANZA | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | ACT; NGO; CBO; FBO |

| NGUZO YA 4<br>MABADILIKO YA MFUMO WA KIMKAKATI WA KILIMO KWANZA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **SHUGHULI** | **MAJUKUMU** | **MUDA** | **MHUSIKA MKUU** | **WAHUSIKA WENGINE** |
| 4.1 | Kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya vyakula muhimu ili nchi ijitosheleze kwa chakula | 1. Kuandaa mipango ya uzalishaji wa mazao ya chakula muhimu kama vile mahindi, mihogo, mpunga, jamii ya maharage, samaki, nyama na bidhaa za maziwa, ngano, ndizi, viazi mviringo, ulezi na mtama. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | ARDHI; MIFUGO; MAJI; VIWANDA; TAMISEMI TPSF |
| | | 2. Kuanzisha utaratibu wa kuchanganya mihogo katika usagishaji wa mahindi na ngano. | Desemb a 2009 | KILIMO | VIWANDA; TAMISEMI; TPSF |
| 4.2 | Kubainisha maeneo ya kipaumbele ya uzalishaji wa mazao yanayoweza kuboresha kilimo haraka kwa kutumia gharama na utaalam mdogo na kukidhi mahitaji ya soko la ndani/nje na kuongeza ajira. | Kuweka na kutekeleza mipango ya kugharamia uzalishaji wa pamba, alizeti, katamu, ufuta na mawese. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | TAMISEMI; ARDHI; TPSF |
| 4.3 | Kubainisha maeneo ya kipaumbele na uzalishaji wa mazao ya kilimo cha bustani (horticulture) | Kuweka mipango ya uzalishaji mazao kama vitunguu, embe, zabibu, maparachichi, mananasi, ndizi, nyanya mboga na viungo. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | TAMISEMI; TPSF; TIB |
| 4.4 | Kubainisha maeneo ya kipaumbele ya uzalishaji mazao yenye ongezeko kubwa la thamani kama vile nyuzi, mimea ya nishati n.k. | Kuweka mipango kwa ajili ya uzalishaji wa mkonge, miwa, mtama mtamu na mbegu za mafuta kwa ajili ya nishati na bidhaa nyingine zilizoongezwa thamani. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | TAMISEMI; TPSF |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4.5 | Kuanzisha Kamati ya Ushauri kuhusu Mabadiliko ya Mfumo wa Kilimo. | Kuunda Kamati ya Ushauri inayojumuisha Sekta Binafsi kushauri maeneo ambayo shughuli mbalimbali katika Mabadiliko ya Mfumo wa Kilimo zitafanywa. | Desemba 2009 | KILIMO | ARDHI; MIFUGO; VIWANDA; TAMISEMI; MAJI; TPSF |
| 4.6 | Kufanya uchambuzi wa mlolongo wa mazao yaliyopewa kipaumbele | Kufanya uchambuzi wa mlolongo wa mazao yaliyopewa kipaumbele kwa kuangalia maeneo nyeti pamoja na jinsi ya kuwaunganisha na kuwashirikisha wazalishaji wa mazao ya kilimo na wasindikaji. | Kuanza Agosti 2009 | TUME MIPANGO | ARDHI; KILIMO; MIFUGO; MAJI; VIWANDA; TAMISEMI |
| 4.7 | Kutunga sheria ya kuboresha Mfumo wa Kilimo cha Mkataba (Contract Farming System - CFS) | 1. Kuharakisha utungaji wa Sheria ya Mfumo wa Kilimo cha mkataba.<br>2. Kuweka misingi ya kujenga uwezo wa wadau wanaojihusisha na Kilimo kwa Mkataba (CFS) | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | SHERIA; TPSF |

# NGUZO YA 5
# ARDHI KWA AJILI YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 5.1 | Kurekebisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999. | 1. Kurekebisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999 ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa uwekezaji wa KILIMO KWANZA. | Ifikapo 2010 | ARDHI | TAMISEMI |
| | | 2. Kuimarisha uwezo wa Maafisa Ardhi wa Wilaya na Halmashauri za Wilaya kutekeleza majukumu yao yanayohusu ardhi. | | | |
| 5.2 | Kuharakisha mfumo wa upatikanaji ardhi | 1. Kuhimiza utekelezaji wa sheria kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi vijijini na mipango miji kufanya michakato itakayojumuisha utoaji wa hati miliki. | Ifikapo 2010 | ARDHI | TAMISEMI |
| | | 2. Kutenga ardhi kwa ajili ya mazao na mifugo na kutangaza maeneo hayo katika Gazeti la Serikali. | Kuanza Agosti 2009 | ARDHI | TAMISEMI |
| | | 3. Kutenga rasilimali za kutosha kwa Halmashauri za Wilaya/Miji ziweze kutekeleza shughuli zilizopangwa kuhusiana na ardhi. | Ifikapo 2010 | ARDHI | TAMISEMI |
| | | 4. Kujenga uwezo wa Ofisi za Ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zisimamie ipasavyo masuala ya ardhi na kuimarisha usimamizi wa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya. | | | |
| | | 5. Kupitia upya gharama za upimaji wa ardhi kwa ajili ya utoaji wa Hati za Usajili. | Desemba 2009 | ARDHI | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5.3 | Kuharakisha utatuzi wa migogoro ya ardhi. | 1. Kuanzisha mifumo ya uharakishaji wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. | Mwisho 2010 | ARDHI | |
| | | 2. Kutenga fedha kwa ajili ya kuharakisha hukumu katika mfumo wa Mahakama (kugharamia watumishi). | | | |
| | | 3. Kuanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji na kuimarisha yaliyopo ili yajihusishe na utatuzi wa migogoro ya ardhi. | | | |
| 5.4 | Kuboresha muundo katika usimamizi wa ardhi | Kupitia na kuboresha utaratibu uliopo wa kugawa ardhi | Ifikapo 2010 | ARDHI | TAMISEMI |
| 5.5 | Kuingiza maeneo yanayofaa kwa kilimo katika mipango ya maendeleo ya miji. | Mipango ya maendeleo ya miji kutambua na kujumuisha maeneo ya kilimo. | Ifikapo 2010 | ARDHI | |
| 5.6 | Kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo (Land Bank) | 1. Wakuu wa Mikoa kutenga maeneo maalum ya ardhi (Land Bank) kwa ajili ya uwekezaji, uzalishaji na biashara. | Mwisho 2009 | OWM | WAKUU WA MIKOA ARDHI; KILIMO; |
| | | 2. Kubainisha na kuweka kumbukumbu za ardhi isiyotumika vizuri kwa ajili ya uwekezaji wa Kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | ARDHI | TAMISEMI |
| | | 3. Kuandaa hatua na taratibu za kisheria zitakazoviwezesha vijiji na wanakijiji kutumia ardhi kama hisa kwa shughuli za ubia na wawekezaji. | | | |
| | | 4. Kupitia upya haki miliki za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili kuwezesha Watanzania kuingia ubia katika uwekezaji unaohusu ardhi. | Kuanza Agosti 2009 | OWM | ARDHI; TIC |
| | | 5. Kuandaa mfumo wa kutathmini ardhi utakao onyesha thamani yake halisi kwa madhumuni ya uwekezaji. | Desemba 2009 | ARDHI | |
| | | 6. Kuhimiza matumizi ya sheria ili kujiepusha na kuhodhi na ulanguzi wa ardhi. | Ifikapo 2010 | ARDHI | |
| 5.7 | Kutumia kwa ukamilifu ardhi ambayo hivi sasa inamilikiwa na Serikali na Taasisi za Serikali. | Kutumia kikamilifu ardhi ambayo inamilikiwa na Serikali na Taasisi za Serikali kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo. | Ifikapo Mwisho wa 2009 | OWM | ARDHI; TAMISEMI |

# NGUZO YA 6
# VIVUTIO KWA AJILI YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 6.1 | Kuainisha vivutio vya sera ya kodi na vivutio vingine ili kuchochea maendeleo ya KILIMO KWANZA. | Kuanzisha Kamati Maalum kupitia na kupendekeza vivutio muhimu, ikiwa ni pamoja na sera ya kodi na vivutio vingine ili kuchochea maendeleo ya KILIMO KWANZA | Agosti 2009 | FEDHA | KILIMO; ARDHI; MIFUGO; MAJI; VIWANDA; TAMISEMI TNBC; TIC |
| 6.2 | Kubuni na kutekeleza hatua za kuimarisha ushindani wa kilimo cha Tanzania. | Kupitia gharama za kufanya biashara katika sekta ya kilimo ili kuiwezesha kuwa ya ushindani zaidi. | Desemba 2009 | TUME YA MIPANGO | TNBC; TPSF |
| 6.3 | Kuondoa vikwazo vya masoko kwa mazao ya kilimo | 1. Kuongeza mtaji kuwezesha Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa kusimamia bei za mazao ya chakula na kuifanya Serikali iwe mnunuzi mkuu wa kutegemewa na kwa bei za soko huria. | 2009/10 | VIWANDA | FEDHA; KILIMO; MAMBO YA NDANI; TAMISEMI; SM. |
| | | 2. Kuongeza uwezo wa Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) kununua mazao kwa kiwango kikubwa na kukihifadhi. | | | |
| | | 3. Kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika ununuzi na uhifadhi wa mazao ya chakula. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | KILIMO; TPSF |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 4. Kuhifadhi akiba ya chakula cha miezi 6 hadi mwaka 1 ili kuhakikisha akiba ya chakula na mwenendo wa bei ni wa kuridhisha.<br>5. Kuondoa vikwazo vya mipaka kwa mauzo ya mazao ya chakula. | Inaende-lea | VIWANDA | KILIMO |
| 6.4 | Utumiaji wa vipimo na viwango halali katika biashara uimarishwe. | 1. Taratibu na sheria za kuuza mazao kwa uzito na vipimo vinavyotakiwa zizingatiwe; (Kutotumia lumbesa, pakacha au sado, n.k.)<br>2. Vyombo vya sheria kutekeleza taratibu na kanuni za uwekaji madaraja (grading) na ufungashaji (packaging) wa bidhaa za kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | MAMBO YA NDANI |
| 6.5 | Kuanzisha chombo cha kuendeleza mazao mchanganyiko. | Kuanzisha chombo cha kuendeleza na kusimamia uzalishaji na masoko ya mazao ya mchanganyiko. | Desemba 2009 | KILIMO | SHERIA |
| 6.6 | Kuboresha bei za mazao | Kuanzisha utaratibu wa kuboresha bei za bidhaa za kilimo | 2010 | VIWANDA | FEDHA |

# NGUZO YA 7
# VIWANDA KWA AJILI YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 7.1 | Viwanda kwa ajili ya kushughulikia mahitaji ya wazalishaji wa kilimo. | Kubainisha na kushughulikia mahitaji ya wazalishaji wa kilimo wa Tanzania. | Desemba 2009 | VIWANDA | TPSF |
| 7.2<br><br>7.2.1 | Nyenzo za Uzalishaji wa Kilimo (Backward Linkages)<br><br>Kuongeza uzalishaji na matumizi ya mbolea. | 1. Kuongeza na kuboresha uzalishaji na ubora wa mbolea za kemikali kutoka uzalishaji wa sasa wa Phosphate na NPK unaofanyika Minjingu hadi kufikia tani 300,000 na zaidi kwa mwaka ifikapo mwaka 2010. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | TPSF |
| | | 2. Kutafiti uzalishaji wa mbolea za kemikali zinazotumia Nitrogen kwa kutumia gesi ya asilia inayopatikana nchini. | | | |
| | | 3. Kuongeza huduma za ugani ili kupanua mahitaji na kuhakikisha matumizi sahihi ya mbolea. | Inaendelea | KILIMO | TPSF |
| | | 4. Kuwezesha upatikanaji wa mbolea ya kutosha. | Kila mwaka | KILIMO | FEDHA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7.2.2 | Kuboresha uzalishaji wa mbegu. | 1. Kufanya tathmini ya utendaji wa kampuni zote za mbegu zilizobinafsishwa (TANSEED) ili kukidhi mahitaji ya taifa | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | |
| | | 2. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mbegu ili kukabili matumizi yaliyoshamiri ya mbegu zisizo halisi. | | | |
| | | 3. Kutoa ruzuku inayohusu mbegu bora na zilizoidhinishwa kwa wakulima wadogo. | Kila mwaka | KILIMO | |
| | | 4. Kuwezesha na kuimarisha Taasisi ya Uidhinishaji Mbegu Rasmi Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI) kuwa mdhibiti. | Desemba 2009 | | |
| | | 5. Kutoa hataza kwa matokeo ya utafiti wa mbegu ili kulinda aina za mbegu zinazozalishwa nchini | Desemba 2009 | | |
| 7.2.3 | Kuainisha na kuimarisha uwezo unaohitajika kwa kuendeleza sekta ya mifugo. | 1. Kuimarisha Kituo cha Taifa cha Utovishaji (National Artificial Insemination Centre - NAIC) kilichoko Arusha na kuanzisha vituo vya kuhifadhi na kusambaza mbegu za madume katika mikoa yote. | Desemba 2010 | MIFUGO | TPSF |
| | | 2. Kufufua na kuanzisha vituo vya uzalishaji mifugo na mitamba. | | | |
| | | 3. Kuhakikisha uzalishaji wa kutosha wa dawa na vyakula vya mifugo hapa nchini. | | | |
| | | 4. Kukarabati viwanda vyote vya maziwa vilivyopo nchini na kuanzisha vituo vya kukusanyia maziwa. | | | |
| 7.2.4 | Kuainisha na kuimarisha uwezo unaohitajika kwa kuendeleza sekta ya uvuvi | 1. Kuwekeza katika nyenzo zitakazowezesha matumizi kamilifu ya rasilimali za majini. | Inaendelea | MIFUGO | TPSF |
| | | 2. Kutayarisha na kuwezesha programu ya ufugaji wa samaki kwa kila wilaya. | | | |
| | | 3. Kuimarisha na kupanua vituo vya uzalishaji samaki kwa ajili ya kusambaza vifaranga wa samaki. | | | |
| | | 4. Kuhimiza hatua na taratibu za uhifadhi wa ufugaji wa samaki na kulinda mazingira. | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7.2.5 | Kuongeza uzalishaji wa dawa za kilimo nchini. | 1. Kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa za kilimo nchini. | Inaendelea | VIWANDA | |
| | | 2. Kuhimiza usimamizi na uangamizaji wa wadudu na wanyama waharibifu. | Inaendelea | KILIMO | |
| | | 3. Kuelimisha wakulima kuhusu masharti na matumizi sahihi ya dawa za kilimo. | | | |
| 7.2.6 | Uzalishaji wa zana na vifaa vya kilimo | 1. Viwanda vya zana za kilimo vilivyo binafsishwa vizalishe vifaa vya kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | |
| | | 2. Kuanzisha uzalishaji wa mashine, vifaa na zana za kilimo nchini | | | |
| | | 3. Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya sekta ya kilimo katika ngazi ya Afrika Mashariki. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | |
| 7.3 | <u>Utunzaji, Usindikaji na Uuzaji wa mazao ya kilimo (Forward linkages):</u> | 1. Kuimarisha sera na taratibu za kukataza usafirishaji mazao ghafi nchi za nje na kuongeza ushuru kwa bidhaa shindani zinazoagizwa toka nchi za nje na kufanya tathmini ya mara kwa mara. | July 2010 | VIWANDA | FEDHA; KILIMO |
| 7.3.1 | Upanuzi wa viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya kilimo. | 2. Kutunga sheria kali ili kuzuia bidhaa za kilimo zilizosindikwa au kuchakatwa kwa kiwango cha chini kuletwa nchini. | Inaendelea | VIWANDA | OWM; TPSF |
| | | 3. Kuendesha kampeni ya "Nunua Bidhaa za Tanzania" kuanzia na manunuzi ya Serikali. | | | |
| | | 4. Kurudisha umiliki na kufufua viwanda vya kusindika au kuchakata mazao ya Kilimo vilivyo binafsishwa ambavyo havijafanya kazi mpaka sasa (viwanda vya korosho, ngozi, nguo n.k.) | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | |
| | | 5. Kuwasaidia na kuwaunga mkono wasindikaji na wachakataji mazao ya kilimo kwa kuwapa vivutio na misaada mingine. | | | |
| | | 6. Kuisaidia SIDO kupanua usindikaji na uchakataji mazao ya kilimo. | | | |
| | | 7. Kuanzisha viwanda vya ufungashaji vya kiwango cha juu kukidhi ongezeko la mazao ya kilimo yaliyosindikwa na yaliyochakatwa. | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7.3.2 | Usimamizi wa kupunguza upotevu na uharibifu wa mazao baada ya kuvuna. | 1. Kuanzisha maghala ya kuhifadhia mazao wilayani. | Kuanza Agosti 2009 | OWM | TAMISEMI; KILIMO |
| | | 2. Kuhimiza uwekezaji wa sekta binafsi katika vifaa vya kuhifadhia mazao yanayoharibika upesi na mazao mengine. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | TPSF |
| | | 3. Kuandaa mkakati wa kuelimisha wakulima njia bora za kuhifadhi na usimamizi wa mazao ya kilimo.<br>4. Kuhimiza uwekezaji katika urutubishaji chakula ili kuboresha lishe. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | TCCIA |
| 7.3.3 | Kuimarisha mkakati wa biashara na usimamizi wake | 1. Kuanzisha vituo vya taarifa za masoko kuwawezesha wakulima kuelewa hali ya biashara katika masoko mbalimbali.<br>2. Kuboresha mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo ili kufikisha kwa wakulima kwa wakati muafaka.<br>3. Kushughulikia matatizo ya wazalishaji ya bidhaa zinazosafirishwa nje.<br>4. Vyama vya wafanyabiashara kuwahamasisha wanachama wao kuanzisha kilimo cha biashara, uzalishaji kwa masoko ya nje, usindikaji na uchakataji wa mazao ya kilimo na usambazaji wa pembejeo. | Kuanza Agosti 2009 | VIWANDA | TPSF;<br>TCCIA |

# NGUZO YA 8

# SAYANSI, TEKNOLOJIA NA RASILIMALI WATU KWA AJILI YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 8.1 | Kuanzisha utaratibu wa kutathmini matumizi yanayokidhi mahitaji ya kisayansi, kiteknolojia na rasilimali watu kwa ajili ya KILIMO KWANZA. | 1. Kufuatilia na kutathmini wataalam wa kilimo waliopo. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | TAMISEMI |
| | | 2. Kuwezesha maofisa ugani kuanzisha mashamba ya mfano na kuwapa wakulima maelekezo ya Kilimo bora. | | | |
| | | 3. Kuweka malengo ya utendaji kwa maofisa ugani kama msingi wa tathmini ya ufanisi wao. | | | |
| | | 4. Kuendesha Mafunzo ya 'Wakulima Wataalam' (Para Professionals) na kuwapeleka katika kila Kata. | Desemba 2009 | KILIMO | TAMISEMI |
| | | 5. Kuimarisha mafunzo kwa wataalam wa udongo na maji. | Inaende-lea | ELIMU | |
| | | 6. Kuimarisha programu ya kuajiri wataalam wa kilimo wakiwemo wahandisi umwagiliaji, wataalam wa maji (hydrologists) wasanifu mabwawa, makandarasi n.k. | Desemba 2009 | KILIMO | KAZI |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 7. Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Wataalamu wa Kilimo | Desemba 2009 | KILIMO | KAZI |
| | | 8. Kuanzisha utoaji mikopo ya kilimo na ugawaji wa ardhi kwa wahitimu wa shahada ya Kilimo wenye sifa ya wajasiriamali. | Ifikapo 2010 | KILIMO | FEDHA; ARDHI; TPSF; TBA; TAASISI ZA FEDHA |
| | | 9. Kulipia mikopo ya gharama zote za masomo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya kilimo. | Ifikapo 2010 | ELIMU | |
| | | 10. Kutayarisha programu ya vivutio ili kuwavutia, kuwafundisha na kuwabakisha vijana katika kilimo. | Ifikapo 2010 | KILIMO | |
| | | 11. Kuingiza masuala ya jinsia katika KILIMO KWANZA na kuandaa programu za kuimarisha nafasi ya wanawake na vijana katika kilimo. | Kuanza Agosti 2009 | KILIMO | JINSIA NA WATOTO |
| | | 12. Kuanzisha vituo vya kutoa huduma na taarifa kama vile za pembejeo, matrekta ya kukodi na taarifa za masoko. | 2010 | KILIMO | TCCIA; ACT |
| | | 13. Asasi za utafiti na mafunzo ya kilimo kutumia kwa ukamilifu sehemu ya mgao wa Serikali wa asilimia 1 ya pato la Taifa (GDP) kwa utafiti na maendeleo. | Inaende-lea | KILIMO | FEDHA; MAWASILIANO; COSTECH |
| | | 14. Kuanzisha vituo vya hali ya hewa katika ngazi ya Kata. | 2010 | MIUNDOMBINU | KILIMO |
| | | 15. Kuanzisha utaratibu wa kuwa na vituo vya kuhifadhia taarifa mbalimbali za kilimo pamoja na masoko. | | VIWANDA | KILIMO; TCCIA |

# NGUZO YA 9
# MIUNDOMBINU KWA AJILI YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 9.1 | Kubaini mahitaji ya uendelezaji miundombinu kwa ajili ya KILIMO KWANZA. | 1. Kujenga miradi ya umwagiliaji ya kutosha kwa kulenga mazao ya kipaumbele, wingi wa mazao na mahitaji ya mahali pa uzalishaji. | Kuanza Agosti 2009 | MAJI | KILIMO |
| | | 2. Kuanzisha uwezo wa kutosha wa kuhifadhi mazao katika ngazi zote kwa mfano uhifadhi kwa majokofu, uhifadhi katika kaya, wilaya na taifa. | Inaende-lea | KILIMO | MIFUGO; MIUNDO-MBINU; TPSF |
| | | 3. Kutekeleza “Mpango Kabambe wa Mamlaka ya Bandari” (TPA Master Plan) unaojumuisha bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Mwambani na Bagamoyo. Vilevile bandari za Maziwa Makuu pamoja na bandari ya nchi kavu ya Kisarawe na uhamishaji wa mizigo baina ya Reli ya Kati na Tazara pale Kidatu. | Kuanza Agosti 2009 | MIUNDOMBINU | TPSF |
| | | 4. Kukamilisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza ili uweze kutumiwa na ndege kubwa. | Kuanza Agosti 2009 | MIUNDO-MBINU | |
| | | 5. Kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mbeya, Iringa na vingine na kuwekeza vifaa vya kuhifadhi mazao ya bustani (maua, mboga na matunda) yanayosafirishwa nje ya nchi. | Ifikapo 2010 | MIUNDO-MBINU | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 6. Kukamilisha mtandao wa mkongo wa mawasiliano wa taifa na kuunganisha na mtandao wa chini ya bahari. | Ifikapo 2012 | MAWASI-LIANO | MIUNDO-MBINU; TANESCO; TRL; SONGAS |
| | | 7. Kuboresha mfumo wa reli na barabara | Inaende-lea | MIUNDO-MBINU | |
| | | 8. Kujenga machinjio ya kisasa na viwanda vya kusindika nyama kila mkoa. | Kuanza Agosti 2009. | MIFUGO | TPSF |
| 9.2 | Vituo vya Soko kwa kila Kata | Kuanzisha vituo vya soko katika ngazi ya Kata na kuviunganisha na vituo vya uzalishaji. | Ifikapo 2015 | VIWANDA | TCCIA |
| 9.3 | Kupeleka Umeme vijijini kwa ajili ya kuboresha Kilimo | Kutenga mtaji wa kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini | Ifikapo 2015 | NISHATI | WAKALA WA UMEME VIJIJINI |

# NGUZO YA 10

# UHAMASISHAJI WA WATANZANIA KWA AJILI YA KILIMO KWANZA

| | SHUGHULI | MAJUKUMU | MUDA | MHUSIKA MKUU | WAHUSIKA WENGINE |
|---|---|---|---|---|---|
| 10.1 | Kuingiza Kilimo KWANZA katika vyombo na mipango ya Serikali | Kuingiza KILIMO KWANZA katika mipango ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. | Agosti 2009 | OWM | KILIMO; ARDHI; MIFUGO; MAJI; VIWANDA; TAMISEMI |
| 10.2 | Kufanya kampeni ya uhamasishaji KILIMO KWANZA katika ngazi ya taifa, mkoa, wilaya kata, na vijiji | 1. Kuchapisha na kuzindua kitabu cha KILIMO KWANZA | Agosti 2009 (Nane nane) | OWM | TNBC |
| | | 2. Kuhamasisha shule na vyuo kushiriki katika kampeni ya KILIMO KWANZA | Inaendelea | ELIMU | TAMISEMI |
| | | 3. Wabunge, Uongozi wa Mikoa na Wilaya kueneza taarifa zinazohusu KILIMO KWANZA. | Agosti 2009 | OWM | TAMISEMI;TNBC |
| 10.3 | Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika KILIMO KWANZA | 1. Kuimarisha ushiriki wa Bekta Binafsi katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA. | Kuanza Agosti 2009 | OWM | HABARI; TPSF |
| | | 2. Kushirikisha vyombo vya habari katika kutangaza KILIMO KWANZA | Inaendelea | MOAT | TNBC |
| 10.4 | Viongozi kushiriki katika kilimo. | Kuhamasisha viongozi katika ngazi zote kujihusisha binafsi katika uzalishaji chini ya KILIMO KWANZA | Kuanza Agosti 2009 | OWM | Viongozi wote |
| 10.5 | Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA | Kutayarisha na kuchapisha taarifa za robo mwaka za maendeleo ya utekelezaji wa KILIMO KWANZA. | Kuanzia Desemba 2009 | OWM | KILIMO; TNBC |

# ORODHA YA UFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ACT | - | Baraza la Kilimo Tanzania |
| BENKI KUU | - | Benki Kuu ya Tanzania |
| CMSA | - | Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| KILIMO | - | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika |
| MAWASILIANO | - | Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia |
| NISHATI | - | Wizara ya Nishati na Madini |
| ELIMU | - | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| MIUNDOMBINU | - | Wizara ya Miundombinu |
| VIWANDA | - | Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko |
| MIFUGO | - | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| ARDHI | - | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi |
| MOAT | - | Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania |
| FEDHA | - | Wizara ya Fedha na Uchumi |
| MAJI | - | Wizara ya Maji na Umwagiliaji |
| KAZI | - | Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana |
| JINSIA NA WATOTO | | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| OWM | - | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| MM | - | Mkuu wa Mkoa |
| TCCIA | - | Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo |
| TIC | - | Kituo cha Uwekezaji Tanzania |
| TNBC | - | Baraza la Taifa la Biashara Tanzania |
| TPSF | - | Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania |
| UTT | - | Mfuko wa Vipande Tanzania |
| HABARI | - | Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo |
| SHERIA | - | Wizara ya Sheria na Katiba. |
| MAMBO YA NDANI | – | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi |
| MAMBO YA NJE | - | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa |
| NGO | - | Taasisi zisizo za Kiserikali |
| CBO | - | Taasisi za Kijamii za Wananchi |
| TBA | - | Chama cha Mabenki Tanzania. |
| FBO | - | Taasisi za Kifedha za Wananchi |
| SM | - | Serikali za Mitaa |
| WIS | - | Wizara na Idara za Serikali |

| | | |
|---|---|---|
| TANESCO | - | Kampuni ya kusambaza Umeme Tanzania |
| HODECT | - | Chama cha Wakulima wa Mbogamboga Tanzania |
| CTI | - | Taasisi ya Wenye Viwanda |
| PPF | - | Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma |
| LAPF | - | Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa |
| GPF | - | Mfuko wa Pensheni wa Serikali |
| NSSF | - | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| PSPF | - | Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali |
| TRL | - | Shirika la Reli Tanzania |